HOTUBA YA MHESHMIWA DKT. HUSSEIN ALI MWINYI, RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA SHERIA ZANZIBAR KWA MWAKA 2024

TAREHE: 07 FEBRUARI, 2024

Mheshmiwa Othman Masoud Othman;
Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar,

Mheshmiwa Hemed Suleiman Abdulla;
Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar,

Mheshmiwa Khamis Ramadhan Abdalla,
Jaji Mkuu wa Zanzibar;

Mheshmiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma,
Jaji Mkuu wa Tanzania;

Mheshmwa Zubeir Ali Maulid;
Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar;

Mheshmiwa Mustapha Siyani,
Jaji Kiongozi wa Mahkama Kuu ya Tanzania;

Mheshmiwa, Mwalimu Haruna Ali Suleiman,
Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria,
Utumishi na Utawala Bora;

Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wote mliopo;

Mheshmiwa Sheikh Hassan Othman Ngwali;
Kadhi Mkuu wa Zanzibar;

Mheshmiwa Dkt Mwinyi Talib Haji;
Mwanasheria Mkuu Zanzibar,

Mheshimiwa Mkurugenzi wa Mashitaka Zanzibar;

Mhandisi Zena Ahmed Said,
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi;

Mheshmiwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini
na Wakuu wote wa Mikoa na Wilaya mliopo;

Mheshmiwa Msajili Mkuu wa Mahkama ya Tanzania;

Mtendaji Mkuu wa Mahkama ya Tanzania;

Mheshmiwa Mrajis wa Mahkama Kuu ya Zanzibar,

Mtendaji Mkuu wa Mahkama ya Zanzibar;

Wakuu wote wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama mliopo,

Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu
wakuu wa Wizara mbali mbali za Serikali mliopo;

Raisi wa Chama cha Mawakili Zanzibar;

Wakuu wote wa Taasisi za Serikali na Binafsi mliopo,

Waheshmiwa Naibu Warajis, Mahakimu, Makadhi, Wakurugenzi,

Viongozi na wafanyakazi wote wa Mahkama mliopo;

Viongozi wote wa Dini mliopo;
Wageni waalikwa wote, Waandishi wa habari,

Ndugu Wananchi,

Mabibi na Mabwana;

ASSALAM ALEIKUM

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na utukufu kwa kutupa neema ya uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana katika Maadhimisho haya ya siku ya Sheria, mwaka, 2024. Nimeelezwa kuwa, haya ni maadhimisho ya 13 ya Siku ya Sheria tokea Mahkama ya Zanzibar na washirika wake kuanza kuadhimisha rasmi siku hii mwaka 2013. Natoa shukrani zangu kwako Mheshmiwa Jaji Mkuu wa Zanzibar kwa kunialika kwa mara nyengine kuwa Mgeni Rasmi kwenye maadhimisho haya. Nasema ahsante sana Mheshmiwa Jaji Mkuu.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa waalikwa wote kutoka Tanzania Bara ikiwa ni pamoja na Mheshmiwa Jaji Mkuu wa Tanzania Prof. Ibrahim Juma na ujumbe wako kwa kuja kuungana nasi kuhudhuria kwenye maadhimisho haya. Kwa hakika, kuwepo kwenu hapa, kunadhihirisha ushirikiano mzuri uliopo kati ya Mahkama ya Zanzibar na Mahkama ya Tanzania na pia ni kielelezo cha mahusiano ya karibu na ya kindugu ya wananchi wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nikushukuruni sana na karibuni sana. Kadhalika, napenda kuwashukuru wageni waalikwa wote pamoja na wananchi walojitokeza kuhudhuria kilele cha Maadhimisho ya

siku ya Sheria hapa Zanzibar pamoja na shughuli mbali mbali zilizoandaliwa katika kuadhimisha sherehe hizi.

Mheshmiwa Jaji Mkuu na washiriki wote,

Ninaelewa vizuri kuwa, maadhimisho haya ya siku ya sheria kikawaida, huashiria kumalizika kwa mapumziko ya Mahkama (Court vacation) na kuanza kwa mwaka mpya wa shughuli za Mahkama. Mapumziko hayo ya Mahkama huanza Disemba 10 na kumalizika Januari 20 ya kila mwaka. Nimefarijika kusikia kuwa, baada ya mapumziko hayo, Mahkama na washirika wake hupata fursa ya kukaa pamoja na kujadili mafanikio na changamoto katika kutekeleza majukumu yao na kupanga mikakati ya kuboresha utendaji kazi wao sambamba na kurekebisha madhaifu ama changamoto zao kwa mwaka mpya wa utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshmiwa Jaji Mkuu na Washiriki wote,

Nimefurahi kusikia kuwa, maadhimisho haya yalitanguliwa na shughuli mbali mbali kama vile Mheshimiwa Jaji Mkuu kuzungumza na Waandishi wa habari juu ya maadhimisho ya Siku ya Sheria kwa mwaka 2024, utowaji wa zawadi kwa vinara wa usimamizi wa haki na wafanyakazi wengine wa Mahkama, utoaji wa elimu maskuli na kwa wananchi katika maeneo mbali mbali na kupitia vyombo vya habari na kuwaaga wastaafu wa Mahkama. Vile vile, kulikuwa na matembezi ya siku ya sheria yaliyombatana na

huduma za uchangiaji wa damu hospitalini na utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi. Nakupongezeni sana kwa shughuli hizo. Nakupongezeni sana kwa ubunifu wenu wa mwaka huu wa kuchangia damu katika hosiptali zetu kwani katika kipindi hiki, mahitaji ya damu katika hospitali zetu yamekuwa makubwa.

Mheshimiwa Jaji Mkuu na washiriki wote;

Napenda kutoa pongezi kwa ubunifu wa Kauli mbiu ya mwaka huu ya maadhimisho haya ya siku ya Sheria isemayo;

'MAZINGIRA BORA YA KAZI, MAADILI, UWAZI NA UWELEDI HURAHISISHA UPATIKANAJI WA HAKI, HUVUTIA UWEKEZAJI NA UKUWAJI WA UCHUMI.'

Kwanza kabisa, kauli mbiu hii inaonyesha ni jinsi gani mnavyohusisha jukumu lenu la usimamizi na utowaji wa haki na maendeleo ya uchumi wa Taifa. Inaonyesha pia, ni jinsi gani Mahkama na Taasisi nyengine za Sheria zinavyotilia maanani uchumi wa buluu katika utekelezaji wa majukumu yao, uchumi ambao ni kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Nane.

Tunapaswa kufahamu kuwa, hivi sasa nchini mwetu kumekuwa na ongezeko la wawekezaji ambao wanawekeza katika sekta mbali mbali zikiwemo ujenzi wa mahoteli, viwanda na miradi mingine ya kiuchumi

Aidha, Serikali inatekeleza miradi mbali mbali ikiwemo miradi mikubwa ya kimkakati. Utekelezaji wa mambo yote hayo lazima uwende sambamba na kuwepo kwa mifumo mizuri ya upatikanaji wa haki itakayohakikisha kuwa, haki inapatikana kwa haraka na kwa uwazi, kwa urahisi na kwa ubora wa hali ya juu. Mwekezaji yoyote huvutika kuwekeza kwenye nchi ambayo mifumo yake ya upatinaji wa haki ina sifa nilizozitaja. Katika eneo hili la upatikanaji wa haki kwa haraka, Serikali inasisitiza sana juu ya matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro (Alternative Dispute Resolution Mechanism) kwani hurahisisha umalizikaji haraka wa mashauri pamoja na kuondoa uaduwi kwa wahusika kwani humfanya kila mhusika kuwa mshindi wa kesi (win - win situation). Hivi sasa tayari, Serikali imeshaanza mchakato wa kuandaa Rasimu ya Sheria ya Njia mbadala za Utatuzi wa Migogoro (ADR ACT). Hivyo, kupitia hadhira hii, naziagiza Taasisi husika za Sheria kuhakikisha kuwa, mchakato wote wa uandaaji na utungaji wa Sheria hiyo unakamilika ili Sheria hiyo ianze kazi ndani ya mwaka huu wa 2024.

Mheshmiwa Jaji Mkuu na Washiriki wote;

Kauli mbiu ya maadhimisho haya ya siku ya sheria imekusanya pamoja mambo manne ambayo ni Mazingira bora ya kazi, Maadili, Uwazi na Uweledi kama msingi mkuu wa kurahisisha upatikanaji wa haki. Napenda nieleze, hatua ambazo Serikali inaendelea kuzichukua za kuimarisha mhimili wa Mahkama na Taasisi zote za Sheria ili ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi, na kwenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya

Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 – 2025, Ajenda ya Maendeleo ya Taifa kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 (ZDV - 2050) na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021 - 2026.

Serikali, imekuwa ikichukua hatua mbali mbali za kuziwezesha Taasisi za Sheria ikiwemo Mahkama kufanya kazi zake kwa uweledi, uwazi na ufanisi wa hali ya juu pamoja na kujenga mifumo rafiki ya upatikanaji wa haki kwa wananchi wote. Ujenzi wa majengo saba (7) ya Mahkama ambao tayari umeshaanza katika Mikoa na Wilaya ya Zanzibar, Ongezeko la Majaji, Mahakimu na Makadhi na Maslahi bora kwa Waheshimiwa Majaji, Mahakimu, Makadhi na watumishi wengine wa Taasisi za Sheria ni miongoni mwa jitihada za Serikali zenye lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya muhimili huu muhimu wa Serikali.

Mheshmwa Jaji Mkuu na Washiriki wote;

Serikali inatambua kwamba, utekelezaji wa sheria kwa uadilifu, uweledi na uwazi na kuwepo kwa mifumo imara ya upatikanaji haki, vina umuhimu mkubwa katika kujenga na kukuza imani ya wananchi kwa Serikali yao, kuleta amani na utulivu katika nchi yetu pamoja kuchochea mafanikio ya kiuchumi, kibiashara na kiuwekezaji.

Ustawi bora wa wananchi wetu, pamoja na mambo mengine, kwa kiasi kikubwa, utategemea kuwepo kwa misingi imara ya kuheshimu haki za binaadamu, utawala bora, uhuru wa Mahkama pamoja na sheria madhubuti zinazoilinda jamii dhidi ya aina zote za unyanyasaji. Hali hiyo ni pamoja na kuwepo kwa mifumo bora ya kimahkama inayoangazia kutafasiri Sheria ipasavyo, kutoa maamuzi ya kiutawala na utekelezaji ili kulinda haki za wanyonge. Vile vile, kuhakikisha kuwa mashauri yote yanayofikishwa Mahkamani yanasikilizwa na kuamuliwa kwa haraka na kwa haki bila upendeleo ili kuondoa malalamiko kutoka kwa wananchi.
Katika eneo hili, niipongeze Mahkama kwa kuanza mchakato wa kuboresha mfumo wa kielektroniki wa usikilizaji wa mashauri kwa msaada wa kitaalamu kutoka Mahakama ya Tanzania.

Aidha, nitowe wito kwa Mahkama kwamba, kwa vile hatimae mifumo yote ni mali ya Serikali, basi pia, kuna haja kubwa ya kuishirikisha Ofisi ya Wakala wa Serikali Mtandao katika mchakato huo. Niwahakikishie kuwa, Serikali ipo tayari kutatua changamoto zote zitakazojitokeza katika kutekeleza azma hiyo ya kuleta mageuzi katika utendaji wa mahakama zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Jaji Mkuu na Washiriki wote;
Kama mnavyoelewa dhamira ya Serikali ni kujenga Uchumi wa buluu na kuongeza ajira kwa vijana wetu. Serikali ya imedhamiria kujenga uchumi utakaowasaidia wananchi wa Zanzibar kuondokana na umasikini. Ndio

maana tunaendelea kuvutia uwekezaji, kuimarisha utalii na kuongeza mapato ya Serikali kwa kuziba mianya yote ya ubadhirifu na ukwepaji kodi pamoja na kupeleka nguvu kubwa kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati.

Ni dhahiri kuwa, kufanikiwa kwa dhamira na mipango ya Serikali ya kukuza uchumi wetu lazima kuende sambamba na mchango mkubwa wa Sekta ya Sheria ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa mifumo mizuri ya upatikanaji wa haki itakayowavutia wawekezaji kutoka nje kuwekeza vitega uchumi vyao hapa kwetu.

Napenda kutumia fursa hii kwa mara nyengine kumpongeza Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Zanzibar kwa kusimamia vyema marekebisho/maboresho kwenye mhimili wa Mahkama. Zaidi ya hayo, vile vile nampongeza Mheshmiwa Mwalimu Haroun Ali Suleiman Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa maelekezo na usimamizi wake mzuri kwa Taasisi zote za Sheria pamoja na kuunga mkono dhana hii ya kuwepo kwa mifumo ya kimahkama inayoakisi kwa pamoja mahitaji ya wananchi, ushirikiano na wadau na Taasisi mbali mbali za Kitaifa na Kimataifa, sambamba na malengo ya uchumi wa buluu na uwekezaji hapa Zanzibar.

Mheshmiwa Jaji Mkuu na Washiriki wote;

Katika salamu zake Mheshmiwa Jaji Mkuu wa Zanzibar, ameeleza kwamba, agizo langu la kuundwa kwa Mahkama Maalum ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi limeanza kufanyiwa kazi na kwa sasa Rasimu ya Sheria hiyo imeshaandaliwa. Kwa mnasaba huo, naziagiza kwa mara nyengine Taasisi zote husika za Sheria kuhakikisha kuwa, mchakato wa utungaji wa Sheria hio unakamilika na Mahkama hiyo ikiwezekana ianze kazi ndani ya mwaka huu.

Aidha, nimefurahi kusikia kwenye salamu za Jaji Mkuu kuwa kumeshaandaliwa Rasimu ya Muongozo wa Urejeshaji Mali Serikalini zinazopatikana kutokana na vitendo vya uhalifu. Hiyo ni hatua nzuri ambayo itahakikisha kuwa, wahalifu hawanufaiki na mapato waliyoyapata kwa njia haramu na ni kigezo kizuri cha namna Serikali ilivyodhamiria kupambana na vitendo vya ufisadi na uhujumu wa mali ya Umma.

Mheshimiwa Jaji Mkuu na Washiriki wote,

Napenda nitumie fursa hii kama kauli mbiu yetu invyoeleza kukumbusha umuhimu wa kuzingatia maadili hususan kwa Waheshimiwa Majaji, Mahakimu na Makadhi wanapokuwepo kazini na nje ya majukumu yao. Sote tuelewe kwamba, miongoni mwa mambo yanayodhoofisha misingi ya utawala bora ni kuwepo kwa vitendo vya ukiukaji maadili kama vile rushwa, ubadhirifu, uzembe, kukosa uwajibikaji, upendeleo katika utowaji wa huduma na matumizi mabaya ya madaraka.

Nimepata faraja kusikia kwenye salamu za Jaji Mkuu, kwamba sasa, uongozi wa Mahkama unachukuwa hatua stahiki kwa watumishi pamoja na Mawakili wa kujitegemea wanaokiuka maadili ya kazi zao. Hongereni sana.

Mheshmiwa Jaji Mkuu na washiriki wote;

Ushirikiano kati ya Mahkama na washirika wake (stake holders cooperation) ni miongoni mwa mambo muhimu katika maboresho ya Mahkama. Napenda nieleze kuwa, uhuru wa Mahkama haumaanishi kuwa Mahkama ijitenge. Katika ulimwengu wa kisasa Mahakama na Taasisi zote za Sheria zinapasa kushirikiana na wadau mbali mbali wa kitaifa na kimataifa kwa sharti tu iwe kwa kufanya hivyo hakuathiri jukumu la msingi la Mahkama na Taasisi nyengine za sheria katika usimamizi na utoaji wa haki. Nimefurahi kusikia kuwa Mahkama imekuwa ikishirikiana na wadau mbali mbali wa kitaifa na kimataifa kama vile Benki ya Dunia, Mashirika na Taasisi za kitaifa na kimataifa nakadhalika. Nakupongezeni sana.

Mheshmiwa Jaji Mkuu na Washiriki wote;

Napenda kumalizia hotuba yangu kwa kueleza kuwa, Serikali yenu ni sikivu na nimezisikia vyema changamoto ziliopo ambazo zinathiri utendaji mzuri wa Mahakama yetu. Nawahakikishia kuwa, tutazifanyia kazi changamoto zote zinazozikabili Taasisi za Sheria na Mahkama kwa mujibu wa hali ya fedha itakavyoruhusu.

Naishukuru sana Mahkama na Washirika wake kwa uratibu na maandalizi mazuri ya maadhimisho haya. Kwa ndugu zetu nyote mliotoka nje ya Zanzibar na hata wale wa hapa Zanzibar mliohudhuria sherehe hizi, nakutakieni makazi mema hapa Zanzibar na safari njema ya kurejea nyumbani. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aizidishie nchi yetu amani, umoja na mshikamano na atuwezeshe kuitekeleza mipango yetu ya maendeleo kwa mafanikio zaidi.

MUNGU IBARIKI MAHKAMA

MUNGU IBARIKI ZANZIBAR

MUNGU IBARIKI TANZANIA

Asanteni kwa kunisikiliza